RESET

# AMR MAKUBALIANO YA JUKUMU LA PAMOJA

pennsylvania
DEPARTMENT OF HUMAN SERVICES

www.dhs.state.pa.us

## MAJUKUMU YAKO NI:

- ✓ Kushirikiana na mhudumu wako wa jamii ili kuunda mpango wa jinsi unavyoweza kujitunza (na familia yako) bila kutumia usaidizi wa pesa. Hii inajumuisha kumwandikishia mtoto au mwanandoa usaidizi isipokuwa kama una sababu nzuri ya kutofanya hivyo.
- ✓ Kushirikiana na mhudumu wako wa jamii ili kuweka malengo mapya hali yako ikibadilika, na umwambie unapokamilisha sehemu za mpango wako.
- ✓ Kamilisha hatua zilizoko katika mpango wako (timiza malengo yako) kufikia tarehe ulizojadiliana na mhudumu wako wa jamii.
- ✓ Kuhakikisha kuwa watoto wako wanaenda shuleni.
- ✓ Kushirikiana na Usaidizi wa Muda mfupi kwa Familia Zisizo na Uwezo (TANF) kukusanya sampuli bila mpangilio ukiombwa. Hii inaweza kujumuisha kumpa mhudumu wako wa jamii saa za ajira na za shughuli zinazohusiana na kazi.
- ✓ Kutumia fedha za TANF zilizotolewa kupitia kadi yako ya Electronic Benefits Transfer (EBT) au kadi ya PA ACCESS kwa miamala inayokubalika. Hupaswi kutumia fedha za TANF zilizotolewa kupitia kadi yako ya EBT au PA ACCESS kufanyia miamala ya uhamishaji wa manufaa wa kielektroniki (EBT) katika maduka ya vileo; kasino (kasino za kuchezea kamari, maeneo ya michezo); au maeneo ya burudani ya watu wazima ambapo watumbuizaji wanavua nguo au wanatumbuiza bila nguo.
- ✓ Kutumia pesa za marupurupu maalum unazopokea kulipia vitu au huduma ulizoomba. Ndani ya siku 14 baada ya kupokea pesa, lazima utoe ithibati ya jinsi pesa zilivyotumika.
  - Usipotumia pesa kwa ajili ya vitu au huduma ambazo marupurupu maalum yaliyotolewa kwa ajili yazo na usipotoa ithibati (kama vile risiti) kuwa ulitumia pesa kwa madhumuni haya, huenda ukalazimika kulipa pesa hizo.
- ✓ Kwa ujumla, lazima ufanye kazi au ushiriki katika shughuli zilizoidhinishwa (isipokuwa kama unaruhusiwa kufanya vingine au una sababu nzuri) kwa angalau saa kadhaa zinazohitajika kwa nyumba yako.
- ✓ Kujidumishia afya njema kwako na kwa familia yako ni hatua muhimu ya kuwa huru.
- ✓ Ikiwa wewe ni mjamzito, ni muhimu utimize miadi yote iliyoratibiwa na daktari au kliniki yako.
- ✓ Kukamilisha, kutia sahihi, na kuandika tarehe kwenye AMR iliyotumwa kwako na kuirejesha ndani ya siku 30 za tarehe ya sahihi ya ofisi ya usaidizi wa kaunti (CAO) kwenye AMR.

## MAJUKUMU YETU NI:

- ✓ Kueleza kuwa unaweza kupokea usaidizi wa fedha kutoka Mpango wa TANF kwa jumla ya miaka 5 pekee (miezi 60) katika maisha yako yote. TANF inatoa usaidizi wa muda mfupi hadi wewe na familia yako muweze tena kujikimu. Huenda ukahitimu kwa TANF iliyopanuliwa baada ya kufikisha kikomo cha TANF cha miaka 5 ukitimiza hali maalum.
- ✓ Kueleza kuwa usaidizi wa kulipia utunzaji wa mtoto unapatikana ili uweze kuenda shuleni, kazini, au kushiriki katika shughuli zingine ili kukusaidia kuhitimu kupata kazi.
- ✓ Kueleza ni marupurupu gani maalum ya huduma saidizi kama vile usafiri, utunzaji wa mtoto, na mavazi, unayoweza kupata na kukusaidia kupata karatasi zinazohitajika ili kuhitimu kwa huduma hizo za usaidizi.
- ✓ Kueleza kuwa shughuli zote, ikiwemo zile ambazo unaweza kuanza mwenyewe, lazima ziidhinishwe na idara.
- ✓ Kueleza kuwa lazima uthibitishe angalau utafutaji 3 wa kazi kwa wiki ombi lako linaposubiri kushughulikiwa, au hutastahikia TANF.
- ✓ Kukusaidia kupata vikundi vingine na/au watu wanaoweza kukusaidia kufanikisha mipango yako ili utimize malengo yako.
- ✓ Kueleza njia zingine tunazoweza kukusaidia, kama vile Mpango wa Utetezi wa Ulemavu (DAP), Mkopo wa Pato Lililopatikana kwa Kufanyiwa Kazi (EIC) na njia zingine tunazoweza kusaidia waathiriwa wa dhuluma za nyumbani.
- ✓ Kueleza nafasi za elimu na mafunzo zinazopatikana.
- ✓ Kueleza kuwa unaweza kujitolea kufanya shughuli zinazohusiana na kazi au elimu/mafunzo ikiwa huhitajiki kufanya kazi.
- ✓ Kukupa taarifa kuhusu Mpango wa Usaidizi wa Lishe Saidizi (SNAP), na uwezekano wa kuendelea kupokea SNAP, Medicaid, na usaidizi wa utunzaji wa mtoto ukiacha kupokea TANF kutokana na mapato ya kazi.
- ✓ Kueleza kuwa ukipokea malipo ya muda funge na sasa unatuma ombi la usaidizi wa kifedha katika kipindi hicho hicho, unahitajika kulipa pesa zote au sehemu ya malipo ya muda funge kwa kipindi hicho.
- ✓ Kueleza kuwa unaweza kupata usafiri ili kuenda kwa daktari au kliniki yako.
- ✓ Kueleza kuwa lazima ushiriki katika tiba ya dawa za kulevya au pombe ikiwa utumiaji wa mihadarati unakuzuia kupata au kudumisha kazi.
- ✓ Kueleza kuwa ikiwa wewe au mwanafamilia ana ulemavu wa kimwili au akili au tatizo la afya ya akili linalokuzuia kufanya kazi, tunaweza kukupendekeza kwa shirika linaloweza kukusaidia. Huduma zote zitakuwa za siri.
- ✓ Kueleza kuwa lazima ukamilishe, utie sahihi, na uweke tarehe kwenye AMR uliyotumiwa na uirejeshe ndani ya siku 30 za tarehe ya sahihi ya ofisi ya usaidizi ya kaunti (CAO) kwenye AMR, au wewe na familia yako huenda msistahiki kupata usaidizi wa kifedha.

| Vifupisho vya Mteja | Tarehe | Vifupisho vya Shirika | Tarehe |
|---|---|---|---|
| | | | |

**MPANGO WA KUJISAIDIA MWENYEWE NA FAMILIA YANGU**

**MAKUBALIANO YA JUKUMU LA PAMOJA**

| NAMBARI YA LAINI: | JINA: | | |
|---|---|---|---|
| KAUNTI: | KESI NAMBARI: | NAMBARI YA SIMU: | TAREHE: |

## MUHTASARI WA KESI: Kwa matumizi ya CAO. Mhudumu wako wa jamii atakamilisha hii nawe.

Idadi ya siku za TANF: ____________

Kiwango cha juu zaidi cha elimu ulichokamilisha: ______________________________

Tarehe ya kuzaliwa ya mtoto wako mchanga zaidi: ____________

Wiki za Uzoefu wa Kazi ya Kulipwa ulizokamilisha: ____________

Saa za Huduma kwa Jamii Zinazoruhusiwa kwa wiki: ____________

## MALENGO: Ni aina gani ya kazi ya kujiendeleza au ya mapato utakayotafuta? Ni mafunzo au elimu gani unayoweza kuhitaji?

Muda mrefu:

Hatua za kwanza:

## VIKWAZO VINAVYOZUIA KUTIMIZA LENGO: Hebu tukamilishe orodha kaguzi ya Tathmini ya Utayari wa Kazi.

## HALI YA AJIRA NA MAFUNZO: Hebu tuone ikiwa unazingatia mahitaji ya kazi.

☐ Lazima ☐ Haihusu

## HALI YA USHIRIKI: Hebu tuangelie vikwazo vyako ili kuona jinsi vinavyoathiri uwezo wako wa kushiriki katika shughuli.

Sababu nzuri na maondoleo yamepitiwa na:

☐ Kuidhinishwa ☐ Kukataaliwa ☐ Hayahusiki

Sababu:

## USAIDIZI WA SHIRIKA NA WADHAMINI: Hebu tuone jinsi sisi au shirika lingine linavyoweza kukusaidia.

______________ Vifupisho vya Mteja ______________ Tarehe ______________ Vifupisho vya Shirika ______________ Tarehe

## MPANGO WA KUJISAIDIA MWENYEWE NA FAMILIA YANGU

**MAKUBALIANO YA JUKUMU LA PAMOJA**

| NAMBARI YA LAINI: | JINA: | | |
|---|---|---|---|
| KAUNTI: | KESI NAMBARI: | NAMBARI YA SIMU: | TAREHE: |

### SHUGHULI ZA KUSHIRIKI:

Nini:

Wapi:

Lini:

Saa:

Lazima ushiriki saa ________ za msingi kwa wiki na saa ________ zisizo za msingi kwa wiki.

Nini:

Wapi:

Lini:

Saa:

Lazima ushiriki saa ________ za msingi kwa wiki na saa ________ zisizo za msingi kwa wiki.

### HAKI ZAKO:

Kabla ya manufaa yako kupunguzwa au kusimamishwa, una haki ya kesi yako kukaguliwa upya ili kutambua ikiwa ulikuwa na sababu nzuri ya kutotimiza mahitaji. Uha haki ya kupokea ilani ya hatua kabla ya manufaa yako kupunguzwa au kusimamishwa. Una haki ya kukata rufaa na kuomba kusikizwa kwa haki ikiwa unapinga uamuzi wetu. Manufaa yako yataendelea ikiwa rufaa yako itatiwa muhuri wa posta au kupokelewa ndani ya siku kumi za tarehe ya kutumwa ya ilani inayopendekeza kupunguza au kusimamisha manufaa yako.

### SABABU NZURI:

Sababu nzuri itazingatiwa ikiwa sababu ya kutokamilisha hatua katika Mpango wako wa Kujisaidia Mwenyewe na Familia Yangu inazidi uwezo wako. Mifano ya sababu nzuri ni dhuluma za nyumbani, kutokuwa na utunzaji mzuri wa mtoto, au hitaji la kumtunza mlemavu au mgonjwa.

Ripoti kuhusu mpango huu kwa ______________________ kufikia: __________ __________

Jina la Mfanyakazi — Tarehe — Nambari ya Simu

Nilisoma na kuelewa fomu hii, inayoitwa Makubaliano ya Jukumu la Pamoja (AMR), ninafahamu kuwa lazima nitie sahihi AMR ili nipate usaidizi wa kifedha. Ninafahamu kwamba kutia sahihi kwenye AMR kunamaanisha ninasema nitafanya kile ambacho mpango wa AMR unaniambia nifanye. Ninafahamu kuwa nisipofanya kile ambacho kimo ndani ya mpango, bila sababu nzuri, “adhabu” zilizoko kwenye ukurasa wa 4 wa AMR hii zinaweza kutokea. Ninafahamu kuwa nisipotia sahihi AMR hii - isipokuwa kama nina sababu nzuri - mimi na familia yangu hatutapata usaidizi wa kifedha (62 P.S. 405.3). Ninafahamu kwamba adhabu za kutotia sahihi AMR zimeorodheshwa kwenye ukurasa wa 4 wa fomu hii.

______________________ __________

Sahihi ya Mteja — Tarehe

______________________ __________

Sahihi ya Shirika — Tarehe

__________ __________ __________ __________

Vifupisho vya Mteja — Tarehe — Vifupisho vya Shirika — Tarehe

| ADHABU ZA MAKUBALIANO | |
|---|---|
| **UKIKATAA AU UKIKOSA KU:** | **ADHABU ITAKUWA:** |
| Andaa mpango na mhudumu wako wa jamii na kutia sahihi Makubaliano ya Jukumu la Pamoja (AMR), isipokuwa kama una sababu nzuri ya kutofanya hivyo. | Hutaweza kustahiki kwa usaidizi wa kifedha hadi utie sahihi AMR hii. Ikiwa wewe au mtu mwingine mzima tayari amepokea miezi 60 ya TANF, wewe na familia yako hamtastahiki kwa usaidizi wa kifedha. |
| Tia sahihi AMR uliyotumiwa na uirejeshe ndani ya siku 30 za tarehe ya sahihi ya ofisi ya usaidizi ya kaunti (CAO) kwenye AMR. | Hutastahiki kwa usaidizi wa kifedha ikiwa AMR haijarejeshwa ndani ya siku 30. Ikiwa wewe au mtu mwingine mzima tayari amepokea miezi 60 ya TANF, wewe na familia yako hamstahiki kwa usaidizi wa kifedha. |
| Shirikiana na mahitaji ya kutafuta usaidizi na/au kuthibitisha ubaba, isipokuwa kama una sababu nzuri ya kutofanya hivyo. | Manufaa yako ya usaidizi wa kifedha wa kila mwezi yatapunguzwa kwa asilimia 25. |
| Timiza mahitaji ya kazi, isipokuwa kama una sababu nzuri ya kutofanya hivyo. Hii ni pamoja na, lakini sio tu:<br>• kushiriki katika kazi au shughuli ya kazi ikiwemo elimu na mafunzo;<br>• kuendelea kutafuta kazi na kuwasilisha nyaraka zinazohitajika; na<br>• kukubali na kudumisha ajira iliyopo. | Ukiukaji wa 1 - Hutastahiki kwa angalau siku 30 hadi uonyeshe na udumishe ufuataji kwa kipindi cha angalau wiki moja na baadaye. Ikiwa hujafuata kwa siku 90, familia yako yote itaondolewa kwenye mpango hadi uonyeshe na udumishe ufuataji kwa kipindi cha angalau wiki moja na baadaye.<br>Ukiukaji wa 2 - Hutastahiki kwa angalau siku 60 na hadi uonyeshe na udumishe ufuataji kwa kipindi cha angalau wiki moja na baadaye. Ikiwa hujafuata kwa siku 60, familia yako yote itaondolewa kwenye mpango hadi uonyeshe na udumishe ufuataji kwa kipindi cha angalau wiki moja na baadaye.<br>Ukiukaji wa 3 - Familia yako yote itaondolewa kwenye mpango kabisa. |
| Dumisha mapato na bila sababu nzuri kupunguza saa zako za kazi hadi chini ya saa 20 kwa wiki kwa hiari. | Ruzuku yako itapunguzwa kwa kiwango cha pesa sawa na kile ambacho ungepata ikiwa hungepunguza saa zako kwa hiari. |
| Shiriki katika tiba iliyopo ya dawa za kulevya au pombe ikiwa utumiaji mihadarati unakuzuia kupata au kudumisha kazi. | Hutastahiki kwa mgao wako wa ruzuku ya fedha hadi ushirikiane na mpango wa tiba uliopo. |
| Tuma ombi la vyanzo vingine vya mapato vinavyowezekana. | Hustahiki hadi ukubali kutimiza mahitaji. Ikiwa wewe au mtu mwingine mzima amepokea miezi 60 ya TANF, wewe na familia yako hamstahiki hadi mfuate. |
| Toa ithibati ndani ya siku 14 za jinsi pesa za marupurupu maalum zilivyotumika. | Huenda ukalazimika kulipa pesa hizo ikiwa hukutumia pesa za marupurupu maalum ulizopokea kulipia vitu au huduma ulizoomba. |

Vifupisho vya Mteja ____________ Tarehe ____________ Vifupisho vya Shirika ____________ Tarehe ____________